**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA FUNDI MKUU UJENZI (LOCAL FUNDI IN BUILDING WORKS) UJENZI WA MAJENGO YA CHUO CHA VETA HAI-KILIMANJARO

**Tarehe 17/03/2023**

Kwa kusudi la kuboresha mazingira ya vyuo vya Ufundi Stadi, Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia inatarajia kujenga **Chuo cha VETA wilaya ya Hai** ili kuwawezesha vijana kupata stadi za kujiajiri na kuajiriwa.

Mradi huu unatekelezwa kwa mwongozo wa 'FORCE ACCOUNT' kama ilivyoelekezwa na serikali kupitia miongozo mbalimbali na kusimamiwa na Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule wilaya ya Hai.

Majengo yanayotarajiwa kujengwa ni kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali: Majengo yanatarajiwa kujengwa.

**MAJENGO YANAYOTARAJIWA KUJENGWA**

| NA | AINA YA JENGO | IDADI YA MAJENGO | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1. | Jengo la Utawala | 01 | Ujenzi mpya |
| 2. | Nyumba ya Mkuu wa Chuo | 01 | Ujenzi mpya |
| 3. | Karakana | 03 | Ujenzi mpya |
| 4. | Kibanda cha Mlinzi | 01 | Ujenzi mpya |
| 5. | Jengo la Umeme | 01 | Ujenzi mpya |
| 6. | Jengo la Madarasa | 01 | Ujenzi mpya |
| 7. | Jengo la Choo | 01 | Ujenzi mpya |
| | **JUMLA YA MAJENGO** | **09** | |

Aidha fomu za gharama za ufundi (Labour charges forms),michoro na ramani zinapatikana ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule wilaya ya Hai saa za kazi, ( saa 2.00 asubuhi hadi 9:30 alasiri).

Kwa mujibu wa utekelezaji wa mradi kwa njia ya 'Force Account',Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule wilaya ya Hai kwa kupitia Kamati ya Mradi wa ujenzi- Chuo cha (VETA) anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu kuomba kazi katika fani zifuatazo:



CamScanner

**A): FANI NA MASHARTI/ SIFA MAHSUSI ZA MAFUNDI WAKUU ZINAZOHITAJIKA; SIFA ZA FUNDI MKUU UJENZI(UASHI,KUPAUA,RANGI,UMEME NA BOMBA):**

1) Kwa kuzingatia ukubwa wa kazi hii Fundi mkuu awe na mojawapo ya sifa zifuatazo;Mhandisi wa ujenzi (Civil and or related Civil Engineering), Fundi sanifu ujenzi, Fundi aliyehitimu mafunzo ufundi Stadi Ujenzi (FTC/Diploma and NVA3), Msanifu majengo (Architect) au Mkadiria Majenzi (Quantity Surveyor) mwenye uzoefu wa miaka angalau mitano na awe amewahi kujenga majengo ya serikali. Pia aambatishe cheti cha Shahada au FTC/Diploma/NVA 3, mikataba na hati za malipo kwa kazi alizowahi kufanya pamoja na CV yake.

2) Awe na mafundi wasaidizi angalau wanne **04** wenye fani za Uashi,Kupaua,Rangi,Umeme na Bomba na aambatishe nyaraka za mafundi hao zikionesha uzoefu wa kazi walizofanya pamoja na CV na vyeti vyao.

3) Kwa kuwa hakutakuwa na malipo ya awali kwa fundi mkuu na kwa kuzingatia ukubwa wa kazi hii,lazima fundi mkuu awe na mtaji ili kuwalipa mafundi wake wasaidizi na vibarua watakaofanya kazi hii.

**4)** Awe amewahi kufanya kazi inayofanana na hii kwa Mwongozo wa 'Force Account'na **Lazima aambatishe nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha kuwa ni kweli amewahi kufanya na kukamilisha bila mashaka:**

a) Mkataba wa kazi inayofanana na hii.
b) Hati za malipo ya gharama za ufundi (payment certificate).
c) **Bank statement** ikionesha gharama za malipo ya ufundi aliyolipwa yenye thamani ya kazi alizofanya katika kipindi tofauti tofauti.
d) Barua pendekezwa (Recommendation letter) kutoka kwa Mwajiri wa awali kwa kazi hiyo.

5) Awe na uwezo wa kusoma michoro na kufanya makadirio ya mahitaji (materials).

6) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kujenga kwa tofali aina zote.

7) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kupaua paa za aina mbalimbali katika majengo ya serikali.

8) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kupaua mabati aina zote na kufanya 'brandering &ceiling.

9) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kuweka sakafu za aina mbalimbali (za kawaida, tiles, terrezo n.k).

10) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kutumia mitambo na vifaa mbalimbali vya ujenzi.



CamScanner

11) Mafundi wake lazima wawe na uwezo wa kufanya kazi za usukaji umeme (wiring) na bomba (Plumbing).

12) Fundi mkuu lazima aandae na kuwasilisha Mpango kazi ukielezea shughuli na muda wa utekelezaji wa mradi sambamba na nyaraka nyingine katika tangazo hili.

13) **Fundi mkuu lazima awasilishe bahasha moja yenye bahasha mbili tofauti ambapo bahasha moja itakuwa na nyaraka tajwa katika tangazo hili (bahasha ya vigezo vya ufundi)** na nyingine i**takayokuwa na gharama za ujenzi kwa majengo atakayoomba**.

14) Mwombaji anatakiwa kudurufu (photocopy) nakala ya michoro na mchanganuo wa shughuli za ujenzi(Schedule of labour) kwa **gharama zake mwenyewe** ili kujaza na kuwasilisha.

15) Fundi lazima aombe na kujaza kazi zote (Uashi,Kupaua,Kupaka rangi,Umeme na Bomba) kama ilivooneshwa katika tangazo hili.Fundi ambaye ataacha kujaza kipengele kimojawapo miongoni mwa vipengele tajwa hapo juu maombi yake hayatafanyiwa kazi.

**16) Inasisitizwa kuwa fundi mkuu anatakiwa kujaza gharama za ufundi tu (Labour Charges kwa kazi tajwa na kusudiwa kwa mujibu wa tangazo hili**.

**A) MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI;**

1) Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18.

2) Mwombaji lazima awe na Namba Ya Utambulisho ya Mlipa Kodi(TIN).

3) Mwombaji lazima awe na Akaunti ya Benki iliyo hai.

4) Mwombaji lazima aandike barua ya maombi kwa jina lake na siyo kampuni au jina la Biashara.

5) Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya 'ki-eletroniki' na posta hayatapokelewa.

6) Mwombaji lazima aambatishe barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji/Mtaa.

7) Mwombaji lazima awe tayari kufanya kazi muda wa usiku na siku za mwisho wa wiki itakapolazimika kufanya hivyo.

8) Barua za maombi ziwasilishwe **kwa njia ya mkono Ofisi ya uthibiti Ubora wa Shule Wilaya ya Hai** saa za kazi (**saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 alasiri**) zikiwa zimeandikwa juu ya bahasha kwa herufi kubwa.



CamScanner

9) Fundi mwombaji awe na vifaa vya ujenzi(ndoo,beleshi,majembe,sururu,panga,toroli ) pamoja na vifaa vingine vinavyohitajika katika ujenzi.

10) Fundi mwombaji awe na mashine ya kuchanganyia zege (kazi zote za kuchanganya zitafanywa kwa mashine).

11) Waombaji wote watatakiwa kutembelea eneo la mradi kwa ajili ya utambuzi wa eneo husika.

12) Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **Alhamisi** ,tarehe **23/03/2023** saa **10.00 jioni** na siku ya ufunguzi wa zabuni ni siku ya **Ijumaa** tarehe **24/03/2023** saa **5:00 Asubuhi**.

13) Maombi yatumwe kwa ;

**Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule Wilaya,**
**Wilaya ya Hai,**
**S.L.P 11,**
**HAI.**

Tangazo hili limetolewa na:

MTHIBITI UBORA MKUU WA SHULE (W)
WILAYA YA HAI

Kawau.

**ASTERIA V. KAWAU**
**Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule Wilaya ya Hai**



CamScanner